**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA WAZIRI MKUU**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA**

## TAARIFA KWA UMMA

## BARAZA LA MADIWANI LAPITISHA MAPENDEKEZO YA MPANGO NA BAJETI YA SHILINGI BILIONI 101.74 KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027

Mkutano wa Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela umepitisha mapendekezo ya mpango na bajeti ya **shilingi bilioni 101.74 (Tshs. 101,745,763,300.00)** inayokadiriwa kukusanywa na kutumiwa katika mwaka wa fedha **2026/2027** ikiwa ni ongezeko la asilimia **13.8** ukilinganisha na bajeti inayoendelea ya mwaka wa fedha 2025/2026

Akiwasilisha mapendekezo hayo kwa niaba ya Mkurugenzi wa Manispaa ya Ilemela, Ndg. Herbert Bilia ambaye ni Mkuu wa Divisheni ya Mipango na Uratibu amesema kuwa, kati ya fedha hizo **Shilingi Bilioni 69.21** sawa na **68.03%** ni **ruzuku ya mishahara ya watumishi** kutoka Serikali kuu, **Shilingi Bilioni 14.57** sawa na **14.32 %** ni **ruzuku ya miradi ya maendeleo** kutoka Serikali kuu na wafadhili, **shilingi Bilioni 1.50** sawa na **1.48%** ni **ruzuku ya matumizi ya mengineyo** kutoka Serikali kuu.

Kwa upande wa mapato ya ndani, Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela katika mwaka wa fedha 2026/2027, inakadiria kukusanya jumla ya **shilingi bilioni 16.45** sawa na **16.18%** ya bajeti yote ya Halmashauri. Kati ya fedha hizo **Shilingi Bilioni 12.07 ni mapato yasiyofungwa ambapo 60%** yake yaani **shilingi bilioni 7.24** zitatumika kwa ajili ya **utekelezaji wa miradi ya maendeleo**, na **40%** ya mapato yasiyofungwa yaani **shilingi bilioni 4.83** zitatumika kwa ajili ya matumizi ya kawaida, aidha **shilingi bilioni 4.37** ni mapato fungwa

Katika mwaka wa fedha **2026/2027** vipo vipaumbele **9** vitakavyozingatiwa ambavyo ni; Utawala bora, ukusanyaji wa mapato ya ndani, ulipaji fidia za ardhi, uboreshaji na uimarishaji wa miundombinu sekta ya elimu msingi na sekondari, kuimarisha utoaji wa huduma za afya na hali ya lishe, kuboresha mazingira ya kufanyia kazi, uboreshaji wa masuala ya jinsia na ustawi wa jamii, uwezeshaji wa shughuli za kiuchumi kwa kutoa mikopo ya 10%, uboreshaji na ukarabati wa miundombinu ya afya.



Digitally Signed By Violencea S Mbakile
Mon Jan 26 14:52:20 EAT 2026

Violencea S Mbakile
Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali

**Mkurugenzi wa Manispaa ya Ilemela, S.L.P 735, Mwanza.**
**Simu Na. +255(28) 2981196, Nukushi:+255(28) 2981196, BaruaPepe:md@ilemelamc.go.tz, Tovuti: www.ilemelamc.go.tz**